FRONTRUNNER 007

# FRONTRUNNER EXAM

## DARASA LA SABA - 2021 ⟨7⟩

## KISWAHILI

**Muda: Saa 1 Dakika 40**

**SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO**

1. Umepewa karatasi hii ya maswali na karatasi ya kujibia. Karatasi hii ina maswali 50.
   *i) Jina Lako* ____________________ *ii) Jina la Shule Yako* ____________________

***Soma kifungu kifuatacho kina nafasi 1 - 15. Jaza na majibu sahihi.***

Wanaume ___1___ bado wanashikilia ___2___ mitazamo ___3___ na wakati sasa wanahitaji kubadilika. Kwa mfano, kuna wanaume ___4___ wanawake kama mashine ya ___5___ watoto. Eti mahali ___6___ wanawake ni ___7___ kuwapikia nao wakistarehe. Wanaume kama hao ___8___ waelewe kwamba wanawake wana ___9___ sawa.

| | A. | B. | C. | D. |
|---|---|---|---|---|
| 1. | ambaye | ambayo | ambao | ambayo |
| 2. | kakaka | kikiki | ndindindi | kokoko |
| 3. | iliyoshinda | iliopitwa | iliyopita | iliyopitwa |
| 4. | waonao | wasikio | wasomao | wachekao |
| 5. | kuwasilia | kuzaa | kuwazalia | kuwazalisha |
| 6. | ya | pa | mwa | kwa |
| 7. | ukumbini | nyumbani | sebuleni | mekoni |
| 8. | si lazima | ni mwiko | ni lazima | si mwiko |
| 9. | haki | ukwasi | ufukara | kesi |

Mgeni wa heshima ___10___ alipokelewa kwa ___11___ na kuvishwa ___12___ la maua shingoni. ___13___ jitu la miraba minne na ___14___ tititi kama ___15___.

| | A. | B. | C. | D. |
|---|---|---|---|---|
| 10. | aliposaili | alipowadia | alipowasili | alipokuja |
| 11. | taadhima | hima | majonzi | jitimai |
| 12. | shada | koja | jozi | korija |
| 13. | Alikuwa | Ulikuwa | Kulikuwa | Lilikuwa |
| 14. | cheusi | mweusi | jeusi | jeupe |
| 15. | sufuria | mpingo | mazishi | chungu |

***Kutoka swala 16 hadi 30 jibu kulingana na maagizo***

16. Kanusha: **Amekula na akashiba**
    A. Hajakula akashiba
    B. Hakula akashiba
    C. Hajala wala akashiba
    D. Hajala wala kushiba

17. Ni neno lipi kati ya haya manne yenye maana ya:- Zawadi kwa utumizi bora au huduma bora za kazi
    A. Mchango
    B. Riba
    C. Masurufu
    D. Bahashishi

18. Ni kikundi kipi kinachoonyesha kinyume cha jinsia?
A. Mtetea - koo B. Tembe - pora
C. Jogoo - jimbi D. Ng'ombe - fahali

19. Neno 'pua' limo katika ngeli ipi?
A. I-I B. LI-YA
C. I-ZI D. U-I

20. Teua kivumishi katika sentensi ifuatayo
**Mwalimu aliwazomea wanafunzi watundu jana**
A. Jana B. Watundu
C. Wanafunzi D. Aliwazomea


21. Ni pambo lipi halijaambatanishwa vyema na kiungo chake?
A. Mkufu - shingoni B. Kekee - kiunoni
C. Udodi - miguuni D. Hina - mikononi

22. Chagua sentensi inayoonyesha hali ya kutendwa
A. Tulichekwa na wapinzani wetu
B. Nilimpigia mwenzangu simu
C. Kipofu alielekezwa njia
D. Mwalimu amewafuunza wanafunzi

23. Babu **amelala kingalingali**. Ni nini maana ya usemi uliopigwa kistari?
A. Amelalia mgongo B. Amelala fofofo
C. Amelalia tumbo D. Amelalia ubavu

24. Chagua neno lisilolingana na mengine
A. Wayo B. Kisigino
C. Kifundo cha mguu D. Kisugudi

25. 'Ningekuwa mwalimu ningenunua gari.' Sentensi hii imeandikwa katika wakati upi?
A. Uliopita B. Mtimilifu
C. Tegemezi D. Mazoea

26. Umbo hili huitwa ________

A. Mchemraba
B. Mraba
C. Mstatili
D. Pia

27. Kutokana na kitenzi 'aka' tunapata nomino _____
A. Mwashi B. Akaaye
C. Akama D. Uwakishaji

28. Chagua wingi wa
**'Chungu hiki kina chungu'**
A. Vyungu hivi vina vyungu
B. Chungu hivi vina vichungu
C. Vyungu hivi vina chungu
D. Chungu hivi vina machungu

29. Chagua usemi wa taarifa ufaao wa sentensi
**"Ukienda utasoma," mama alisema**
A. Mama alisema kuwa angeenda angesoma
B. Mama alisema ungeenda utasoma
C. Mama alisema ukienda utasoma
D. Mama alisema kuwa nikienda nitasoma

30. Tegua kitendawili kifuatacho:-
**Babu hupiga kelele anapotabawali**
A. Ngamia B. Mvua
C. Kalamu D. Mtoto

***<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40</u>***

Pendo alizaliwa katika aila ya Bwana Mwema na Bi Zuhura. Malezi yake yakawa ya furaha chungunzima, uchangamfu na fanaka. Wazazi wake walikuwa matajiri tipwa tipwa na wenye mkono wazi katika hara yao.

Bwana Mwema na Bi Zuhura walikuwa wasomi. Kisomo chao hakikukuja hivi hivi iliwabidi kuinamia cha mvunguni ndipo wakafikia walipo sasa. Masomo yao yalikuwa yenye shida belele kwa kuwa lindi hilo la ukata. Alielewa fika kwamba atafutaye hachoki akichoka keshapata.

Pendo alipelekwa katika shule moja iliyomfaa zaidi. Alitangamana na wenzake vyema. Alikuwa na kichwa chepesi kwani alishika mambo haraka haraka. Bidii zake za mchwa zilimfanya kupendwa na kila mmoja. Ni ukweli mtupu wahenga waliposema kuwa chema chajiuza kibaya chajitembeza. Alizidi kuwa bora masomoni mwake.

Upande wa michezo, Pendo alikirimiwa kipawa chema. Alishiriki katika riadha, kandanda na kuingiza. Kila mmoja alimsifu na kummiminia sifa tambi tambi. Je, ni nani asiyeelewa kuwa chanda chema huvikwa pete? Nakumbuka vizuri sana wakati alipopokezwa tuzo kwa kushiriki katika michezo ya kuigiza hadi kiwango cha kitaifa. Aliwahi kumsalimia Rais wetu kwa mkono. Wewe umeshafanya hivyo? Jijibu basi.

Alipofika katika darasa la nane aliukalia mtihani wa kitaifa (K.C.P.E). Matokeo yalipotangazwa alikuwa miongoni mwa waliofanya vyema zaidi si katika shule yake pekee, bali hata katika taifa zima alishikia nambari ya tatu kwa ubora; Mungu akupe nini na akunyime nini? Shukrani kwa Maulana.

Alijiunga na shule maarufu ya sekondari. Alizidi kuchudika hadi alipofanya mtihani wa K.C.S.E ambapo alipata daraja la 'A' sheshe. Alienda katika chuo kikuu na kusomea taalama ya 'udaktari.' Leo hivi ni daktari tajika anayeshughulikia kuunganisha viungo vya mwili vilivyovunjika. Walimwengu wote duniani wanaitegemea taaluma yake kotekote. Amesafiri sana katika nchi za ng'ambo kama vile Marekani na Ujapani kutoa huduma huzo. Naam, mkulima mmoja walaji wengi. Ninampigia upato Pendo kwa idili zake ambazo ni kielezo bora. Sadakta Bwana Mwema na Bi. Zuhura

---

31. Malezi ya Pendo
    A. Yalikuwa na changamoto nyngi
    B. Yalikuwa bora
    C. Yalikuwa ya ati - ati
    D. Yalikuwa na uchangamfu pekee

32. Kisomo cha Bwana Mwema na Bi. Zuhura kilitokana na
    A. Mazingira yalizoleleua
    B. Kipato kikubwa walichokipata
    C. Bidii walizokuwa nazo
    D. Ukuta uliowazonga

33. Kifungu "shida belele" ni tamathali gani ya lugha?
    A. Methali
    B. Nahau
    C. Tanakali
    D. Kitendawili

34. Sifa ipi ni sahihi kwa Pendo alipokuwa shuleni
    A. Alizembea masomoni
    B. Alipendwa na wanafunzi wachache
    C. Alikuwa na bidii na kushika mambo haraka
    D. Alitengana na wanafunzi wote

35. Katika michezo
    A. Alipata tuzo bora
    B. Alicheza kandanda pekee
    C. Alipenda kuwa shabiki sugu
    D. Alishiriki katika riadha hadi kiwango cha kitaifa

36. Jambo lipi lilimfanya msimulizi kushabiki Pendo?
    A. Malezi yake
    B. Tabia njema yake
    C. Kumsalimia rais wake
    D. Kupita mtihani wake

37. Msimulizi anadhamiria nini anaposema "Mungu akupe nini na akunyime nini?
    A. Pendo alikuwa mbaya
    B. Makuzi ya Pendo yalimfurahisha
    C. Wazazi wa Pendo walikuwa wema
    D. Pendo alikuwa na hulka za kupigiwa mfano

38. Taaluma ya pendo ni
    A. Ualimu
    B. Uhunzi
    C. Uhazigi
    D. Unokoa

39. Ni kweli kuwa
    A. Kila mmoja alipendezwa na aila ya Pendo
    B. Taalama ya Pendo ilienea kila mahali
    C. Huduma ya Pendo ilihitajika ulimwenguni kote
    D. Msimulizi alisoma na Pendo

40. Neno jingine lenye maana sawa na Maulana ni
    A. Mwandani
    B. Adili
    C. Mwenzi
    D. Jalali

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali 41 - 50***

Mazingira safi ndio ufunguo wa maisha bora. Tunapoyatunza mazingira yetu kwa kuyalinda na kuzingatia usafi, hutusaidia kuepuka ndwele za kila nui zinazotughasi na kutusababishia maafa chungu nzima. Miongoni mwa yale mambo anayohitaji binadamu ni kuwa na afya njema. Nayo afya njema hutegemea mazingira yaliyotunzwa.

Kwanza kabisa, ni vyema tujiulize swali moja. Je, mazingira ni nini? Mazingira ni hali au mambo yanayomzunguka kiumbe mahali anapoishi. Mazingira huhusisha vitu kama vile mito, maziwa, milima, mabonde, miti, bahari, hewa, mimea na kadhalika. Vitu hivi vyote mwanadamu anavihitaji ili kuyaendesha maisha yake barabara.

Hata hivyo, sisi binadamu wakati mwingine kutokana na uchu wa njenje, wakati tunapojizumbulia riziki ndipo tunapoutekeleza wazimu wa kuyaharibu mazingira. Hatukumbuki kuwa hali hii hutuathiri baadaye na kutuacha tukiangua kilio cha mbwa mdomo juu.

Mwanadamu ana jukumu la kuyatunza mazingira yake kwa kupanda miti ya kutosha na kuhakikisha kuwa ile iliyopo haikatwi ovyo. Miti ikikatwa **kivoloya** kwa kisingizio cha kutafuta mbao za ujenzi, kuni na makaa, itasababisha kuenea kwa jangwa. Aidha tusiyachafue maji ya mito, bahari, maziwa dawa za kemikali kutoka viwandani na makazini. Kitendo hiki huangamiza viumbe wanaoishi majini kama vile samaki ambao ni chakula murua kwa binadamu.

Vile vile, uchafu mwingine wa mazingira ni ule wa kuichafua hewa yetu tunayoitegemea sana. Kuna mitambo mingi inayotoa moshi unaochafua hewa kama vile mashine ya viwandani na ya magari mabovu. Tujiepushe na tabia za kutupa taka shaghala baghala na kusababisha **mirundikano** kila mahali. Tunafaa kuunda majaa ya kutupia taka na kuhakikisha mitaro ya maji machafu inapitisha maji ili yasituame. Tukifanya hivi tutajiepusha na shida nyingi ambazo zingetuzonga. Tunafaa kukumbuka kuwa mwiba wa kujichoma huambiwi pole.

41. Mazingira safi yamelinganishwa na nini?
   A. Afya njema
   B. Kilio cha mbwa mdomo juu
   C. Ufunguo wa maisha bora
   D. Ufunguo wa afya bora

42. Kulingana na kifungu; kuyatunza mazingira na kuzingatia usafi ___________
   A. Hutuepusha maafa chungu nzima
   B. Hutupa afya njema
   C. Hutusaidia kuyaendelesha maisha yetu barabara
   D. Hutusaidia kuepukana na magonjwa yanayotutafisha na kutusababishia masaibu

43. Ni maradhi yapi kati ya haya ambayo hayasababishwi na kutozingatia usafi?
   A. Waba
   B. Homa ya matumbo
   C. Utapiamlo
   D. Tauni

44. Aghalabu binadamu huingiwa na pepo wa kuyabananga mazingira kutokana na ___________
   A. Tamaa ya hela
   B. Kujizimbulia riziki
   C. Shughuli zake za kila siku
   D. Kutaka kutosheleza mahitaji yake

45. Kuangua kilio cha mbwa mdomo juu ni _______
   A. Kulia kwa uchungu
   B. Kujuta
   C. Kuathirika kwa njia Fulani
   D. Kuwa wazimu

46. Mwanadamu ana jukumu lipi kuu zaidi?
   A. Kuipanda miti na kuhakikisha kuwa ile iliyopo haikatwi asilani
   B. Kuyatunza mazingira kwa kupanda miti, kuzuia uchafunzi wa mito na hewa pamoja na kutotupa taka ovyo
   C. Kuyatunza mazingira kwa kuzuia uchafunzi wa hewa na mito pamoja na kuhifadhi vianzo vya maji
   D. Kuyasafisha mazingira yake kila mara ili ajilinde dhidi ya magonjwa

47. Neno kivoloya limepigwa mstari. Neno hilo ni
   A. Kielezi kinachomaanisha 'bila ya mpango'
   B. Kivumishi kinachomaanisa 'kwa haraka'
   C. Kielezi kinachomaanisha 'kwa haraka'
   D. Kivumishi kinachomaanisha 'bila ya mpango'

48. Kitendo kipi cha uchafuzi wa maji ya mito, maziwa na bahari ambacho kina athari kubwa zaidi?
   A. Kutupa taka
   B. Kumwaga dawa za mbolea
   C. Kumwaga dawa kemikali za sumu kutoka viwandani
   D. Kuelekeza maji taka yenye uchafu mwingi

49. Mbali na samaki ni viube gani wengine wanaoishi majini?
   A. Pweza, Kobe, Tohe
   B. Kaa, Lumbwi, Kasa
   C. Lumbwi, Kobe, Pweza
   D. Kasa, Pweza, Kaa

50. Methali ipi nyingine inayoweza kutumiwa badala ya mwiba wa kujichoma huambiwi pole?
   A. Mlimbua nchi ni mwananchi
   B. Mchimba kisima huingia mwenyewe
   C. Msiba wa kujitakia hauna kilio
   D. Mkuki kwa nguruwe kwa binadamu mchungu